**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

# SHERIA YA MTOTO TANZANIA



### 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171.Kwa mujibu wa sheria hii pamoja na mambo mengine Tume inajukumu la kufanya mapitio ya sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa kiuchumi na kitekinolojia.

Katika kutekeleza jukumu hili, Tume imefanya mapitio na Taarifa ya Mfumo wa Sheria Kuhusu Mtoto, 1994.

### 2.0 SHERIA YA MTOTO, SURA YA 13

Kwa kuzingatia mapendekezo ya Taarifa ya Tume mwaka 2009 Serikali ilitunga Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ambayo imeainisha masuala mbalimbali yanayohusu mtoto kama ifuatavyo;

### 2.1 Maana ya Mtoto

Mtoto ni mtu aliye chini ya umri wa miaka kumi na minane (18).

### 2.2 Mtoto na Makosa ya Jinai

Sheria imeweka utaratibu wa kusimamia makosa ya jinai kwa mtoto kwa kuanzisha; mahakama mahsusi kwa watoto, mahabusu; shule za maadilisho, taratibu za uendeshaji mashauri; utoaji wa dhamana na utaratibu wa vipindi vya uangalizi baada ya kuhukumiwa. Mtoto anayetiwa hatiani hapaswi kupewa adhabu ya kifungo isipokuwa adhabu mbadala.

### 2.3 Matunzo ya Mtoto

Sheria inatoa wajibu kwa mzazi, mlezi au mtu yeyote anayetunza mtoto kutoa mahitaji ya chakula, malazi, mavazi, matibabu, elimu, uhuru wa mawazo na haki ya kucheza na kuburudika. Mtu atakayeshindwa kutekeleza wajibu huo anatenda kosa ambapo akitiwa hatiani atapewa adhabu ya kulipa faini ya shilingi milioni tano au kifungo cha miezi isiyopungua sita au vyote kwa pamoja. Jukumu la matunzo ya mtoto litakoma pale mtoto atakapotimiza miaka kumi na nane (18). Matunzo ya mtoto mwenye umri wa zaidi ya miaka 18 yanaweza kuendelea endapo atakuwa anaendelea na masomo au mafunzo.

### 2.4 Ulinzi wa Kisheria wa Makazi ya Mtoto

Sheria inazuia kumnyang'anya mtoto haki ya kufaidi na kufurahia mali ya mzazi wake na kwamba mtoto aliyeasiliwa pia ana haki ya kurithi mali zilizoachwa na mzazi aliyemuasili.

### 2.5 Ulinzi wa Mtoto

Sheria inakataza kumfanyia mtoto ukatili, unyama, vitendo visivyo vya kibinadamu au udhalilishaji unaohusisha matendo ya kimila yanayoondoa utu wa mtu au kuathiri ustawi wa akili na maumbile yake. Mtu anayekiuka masharti haya anatenda kosa ambapo akipatikana na hatia atapewa adhabu ya faini ya Shillingi 5,000,000/ au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

### 2.6 Maeneo ya Starehe

Sheria inazuia mtoto kuingia kumbi za dansi, vilabu vya pombe au klabu za usiku. Pia sheria inakataza mtu kumuuzia mtoto sigara, pombe, madawa ya kulevya au kilevi chochote. Mtu anayekiuka masharti haya anatenda kosa ambapo akipatikana na hatia atapewa adhabu ya faini isiyozidi Shillingi 5,000,000/= au kifungo kisichozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja.

### 2.7 Vitendo vya udhalilishaji

Sheria inakataza udhalilishaji wa kingono kwa mtoto. Mtu yeyote haruhusiwi kumshawishi au kumlazimisha mtoto kuangalia picha za kingono au kufanya shughuli za ngono au vitu vinavyofanana na hivyo. Mtu anayekiuka masharti haya anatenda kosa ambapo akipatikana na hatia atapewa adhabu ya faini isiyozidi 5,000,000/= au kifungo kisichozidi miaka ishirini au vyote kwa pamoja.

### 2.8 Usawa

Sheria inakataza ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya mtoto kwa minajili ya jinsi, rangi, umri, dini, lugha, ulemavu, hali ya afya, desturi, uasili, mazingira ya makazi anakotoka, kuzaliwa, hali ya maisha, ukimbizi au hali nyingine yeyote.

### 2.9 Haki ya Kufanya Kazi

Sheria inaruhusu mtoto mwenye umri kuanzia miaka 14 kufanya kazi nyepesi zisizohatarisha afya, elimu na maendeleo yake. Sheria inazuia kumshawishi, kumlazimisha au kumshurutisha mtoto kufanya kazi kinyume cha sheria. Mtu atakayekiuka masharti haya atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shillingi 200,000/= au kifungo cha miezi 6 au vyote kwa pamoja. Mtoto huyo anahaki ya kupata ujira wa kazi anayofanya

Sheria inakataza ajira za kinyonyaji kwa mtoto na inamtaka kila Mwajiri kuhakikisha mtoto aliyeajiriwa analindwa dhidi ya ubaguzi au vitendo vyenye athari kwake kwa kuzingatia umri na uwezo wake. Mtu anayekiuka masharti haya anatenda kosa ambapo akipatikana na hatia atapewa adhabu ya faini ya shillingi 100,000/= au kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Sheria inamzuia mtoto aliyeajiriwa kufanya kazi usiku kuanzia saa 2 usiku hadi saa 12 asubuhi. Mtu anayekiuka masharti haya anatenda kosa ambapo akipatikana na hatia atapewa adhabu ya faini isiyopungua shilling 100,000/= au kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

### 2.10 Wajibu wa Serikali za Mtaa kwa Mtoto

Sheria inatoa wajibu kwa Serikali za Mitaa kulinda na kutetea maslahi ya mtoto ili kuhakikisha kuwa analelewa katika mazingira stahiki na kwa maadili ya jamii na Taifa. Aidha, Afisa Ustawi wa Jamii ana wajibu wa kushirikiana na Serikali za Mitaa kutoa ushauri na mafunzo kwa wazazi, walezi, ndugu na jamii juu ya ustawi wa mtoto.

### 2.11 Taarifa ya Uvunjwaji wa Haki ya Mtoto

Jamii ina wajibu kutoa taarifa kwa viongozi wa Serikali za Mtaa kuhusu uvunjwaji wa haki ya mtoto unaofanywa na mzazi, mlezi au ndugu.

### 3.0 HITIMISHO

Ulinzi wa haki za mtoto ni jukumu la jamii nzima ili kuhakikisha kwamba mtoto anaishi katika mazingira salama kwa ajili ya ustawi wake kwa kuzingatia Sheria ya Mtoto.


**Kwa maoni wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo:**

**Katibu Mtendaji,**
**Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,**

**Jengo la Taaluma Na. 1,**
**Barabara ya Mkalama**
**S.L.P. 1718**
**DODOMA,**
**TANZANIA**

**Barua pepe: lrct@lrct.or.tz**
**Tovuti: www.lrct.go.tz**